Sauti ya
TUICO

HALIUZWI

TOLEO NA: 24

Toleo la Januari - Machi, 2021

Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa 2016-2020; Mafanikio, Changamoto na Mwelekeo Mpya

- Idadi ya Wanachama yazidi kuongezeka
- TUICO Yafanya Mkutano Wake Mkuu wa Sita
- Mhagama: Vyama vya Wafanyakazi chachu Uboreshaji mazingira ya Kazi

Jenga Chama Imara. Imarisha Mshikamano

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Boniface Y. Nkakatisi
Katibu Mkuu | TUICO TAIFA

Mhariri Mkuu
Venance Majula
Afisa Habari | TUICO

Wajumbe
Samwel Lyimo
Issa Sadallah
Tamim Salehe
Noel Nchimbi
Peles Jonathan
Margaret Ndagile
Fredrick Mng'ong'o
Silpha Kapinga

Msanifu Mkuu
Haji Iddi

YALIYOMO

Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa 2016-2020; Mafanikio, Changamoto na Mwelekeo Mpya 3
Waziri Mhagama: Vyama vya Wafanyakazi Chachu Uboreshaji Mazingira ya Kazi ... 7
TUICO Yashiriki Uzinduzi wa Mpango Kazi Kushughulikia Migogoro ya Kazi Nchini 8
TUICO Yafanya Uchaguzi Mkuu 12
Nguvu ya Mshikamano Katika Kupigania Haki za Mfanyakazi 13
Sangeze: Ni Wakati wa Kuwajibika Zaidi 14
KUT Yajadili Bajeti ya TUICO 2021..... 15

Ilala Sharif Shamba | S.L.P. 5680, Dar es Salaam.
Simu: +255 22 2866910, 2866959/60 | Faksi: +255 22 2866911
Barua pepe: tuico2004@yahoo.com

Info: info@tuico.or.tz | : @tuicounion | : @tuicounion |
: @tuicounion | : TUICO UNION

Jenga Chama Imara. Imarisha Mshikamano

Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa 2016-2020; Mafanikio, Changamoto na Mwelekeo Mpya

TUICO ni Chama huru cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za fedha, Huduma na Ushauri kilichosajiliwa chini ya ofisi ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi Tanzania ambacho lengo lake sio kujipatia kipato au faida bali ni kulinda na kutetea haki, heshima na masilahi ya wanachama wake na wafanyakazi kwa ujumla.

TUICO ilianzishwa kwa malengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya wanachama na wafanyakazi wawapo kazini; kushirikiana na kujadiliana na waajiri katika kuunda kamati za majadiliano na kuanzishwa kwa mabaraza ya wafanyakazi ili kudumisha amani na utulivu mahala pa kazi.

Malengo mengine ni pamoja na kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya mwajiri na mwanachama au mwanachama mmoja na mwingine kwa njia ya makubaliano ya amani kila itakapowezekana; kujadili, kufunga na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya hali bora za kazi, tuzo, kanuni za utumishi na sheria nyingine za kazi zitumikazo nchini. Lakini pia, kushirikiana na vyama vingine vya wafanyakazi nchini pamoja na vile vya kimataifa.

Kama chama cha wafanyakazi, dhamira yetu kwa miaka mitano iliyopita

imekuwa ni kuwaelimisha wanachama kuhusu sheria za kazi na namna ya kutumia taasisi za kazi zilizopo na kusimamia utekelezaji wa sheria husika. Tumeendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wanachama kujua haki na wajibu wao kama wanachama na kama wafanyakazi.

Tumewajengea uwezo viongozi wa TUICO kuanzia ngazi ya tawi (eneo la kazi) hadi taifa sambamba na kuendeleza TUICO inayoongozwa kidemokrasia na yenye kupigania haki, heshima na masilahi ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na haki za kijamii na kiraia katika nchi. Lakini pia, tumeendelea kuwaandaa wanachama wa TUICO wanaokaribia kustaafu kazi ili kuhimili changamoto zinazoambatana na maisha nje ya kazi sambamba na kujenga chama imara, endelevu na chenye nguvu kifedha.

Wanachama

Kama ilivyo kwa vyama katika kada mbalimbali, uhai, nguvu na umoja wa Chama cha Wafanyakazi pamoja na mambo mengine unatokana na idadi ya wanachama na namna wanavyokielewa na kujiunga nacho. Hadi mwezi Juni 2020, TUICO kimerekodi jumla ya wanachama 98,299 ambapo kulingana na jinsi zao; wanaume ni 61,454 na wanawake ni 36,845 wanaofanya kazi katika taasisi za umma na za binafsi kwenye sekta za viwanda, biashara, taasisi za fedha, huduma na ushauri.

Katika kipindi cha Januari 2016 hadi Disemba 2020,

tumefanikiwa kuongeza idadi ya wanachama kutoka elfu sabini na tano, mia tano na sabini na sita (75,576) hadi elfu tisini na nane, mia mbili na tisini na tisa (98,299) ikiwa ni ongezeko la wanachama elfu ishirini na mbili, mia saba na ishirini na tatu (22,723) sawa na asilimia thelathini (30).

Utetezi wa Mashauri na Migogoro

Utetezi wa mashauri na migogoro katika ngazi mbalimbali za maamuzi huwapatia wanachama haki zao lakini pia husaidia kuongeza imani na hamasa ya wafanyakazi kwa vyama vya wafanyakazi. Katika kipindi cha Januari 2016 hadi Disemba 2020, mashauri ya ana kwa ana 1,453 yalipokelewa, 1,361 yalithibitishwa na mengine 93 yanaendelea. Migororo 4,958 ilipokelewa kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), 4,040 ilithibitishwa, 2 haikuthibitishwa na mingine 916 inaendelea.

Migogoro mingine 12 ilipokelewa katika mahakama za Wilaya na Mikoa, 11 ilithibitishwa na 1 bado unaendelea. Migogoro 557 ilipokelewa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, 356 ilithibitishwa, 7 haikuthibitishwa na 194 inaendelea. Migogoro mingine 10 ilipokelewa Mahakama Kuu, 6 ilithibitishwa na 4 bado inaendelea.

Semina na Matawi

Jumla ya semina 7,048 kwa wanachama na wafanyakazi 187,850, mikutano 8,165 kwa wanachama na wafanyakazi 194,495 na ziara 18, 279 za kuwaelimisha viongozi wa matawi, wanachama na watendaji wa ngazi zote, katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini zimefanyika katika kipindi cha Januari 2016 hadi Disemba 2020. Aidha, TUICO tumefanikiwa kuunda matawi mapya kwa zaidi ya asilimia 54, kamati za wanawake na za afya na usalama kazini kwa asilimia 61 na 67 mtawalia. Hali hii imesaidia kuongeza maarifa kwa wafanyakazi kuhusu sheria na kanuni mbalimbali za masuala ya kazi.

Mikataba ya Hali Bora

Kwa upande mwingine, katika kipindi cha Januari 2016 hadi Disemba 2020, tumefunga mikataba 511 ya hali bora kati yetu na makampuni mbalimbali hapa nchini. Mikataba hii husaidia kwa kiasi kikubwa kuleta ustawi wa haki, heshima na masilahi katika maeneo yao ya kazi.

Pia, husaidia kuongeza ufanisi na tija kwa pande zote mbili kwa maana ya mfanyakazi na mwajiri. Mikataba hii imesaidia kuboresha vipato vya wafanyakazi, mazingira ya kazi, lakini pia, TUICO kutambulika mahala pa kazi. Kwa mfano, mwezi Julai, 2019, TUICO ilifunga mkataba wa hali bora na Kampuni ya Sigara (TCC Plc) na Mwezi Agosti 2020, TUICO ilifunga mkataba wa hali bora na kiwanda cha Lake Cement Limited cha Dar es Salaam.

Ushirikiano na Mashirikisho Mengine

Tumeendelea kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) pamoja na mashirikisho ya wafanyakazi ya kimataifa. Kupitia mshikamano huu TUICO kwa kushirikiana na mashirikisho kama vile Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Kimataifa (IndustriALL Global Union); Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi la Uholanzi (FNV); Shirikisho Wafanyakazi wa Viwanda vya Saruji na Mbao (BWI) na PSI, Chama kimepata mifumo ya TEHAMA mfano, mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu na taarifa yaani Management Information System (MIS) na huduma ya intaneti.

Changamoto

Licha ya mafanikio ndani ya kipindi cha miaka mitano, Chama kimekumbama na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto tulizibainisha kwenye Mkutano Mkuu wa Sita wa TUICO Taifa uliofanyika Disemba 29, 2020, mkoani Morogoro.

Katika Mkutano huo uliofunguliwa na Waziri wa Nchi (Ofisi ya Waziri Mkuu), Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama, mjini Morogoro tulitanabaisha changamoto zifuatazo za kisheria zinazojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za Chama chetu na kuitaka serikali izifanyie kazi.

Mosi, **kifungu cha 9(6) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6/2004** kuhusu "senior management employee" ambapo kwa mujibu wa kifungu hicho, wafanyakazi hao wanaweza wasijiunge na vyama vya afanyakazi. Baadhi ya waajiri, wamekuwa wakiwakataza hata wasimamizi (supervisors), makatibu muhtasi, watunza vifaa (store keepers), kujiunga na vyama vya wafanyakazi kwa kigezo cha kuwa nao ni sehemu ya menejimenti.

Pili, ni kuhusu **utatuzi wa migogoro**. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) au Mahakama inaweza kuamuru mfanyakazi aliyeachishwa kazi kurudishwa kazini, lakini bado mwajiri anaweza kuamua kumuachisha mfanyakazi kazi husika kwa kumlipa fidia kama inavyobainishwa katika kifungu cha 40(3) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6/2004.

Tatu, ni **masharti ya usajili wa vyama vya wafanyakazi**; yanaruhusu uwepo wa utitiri wa vyama, na vingine visivyo na malengo wala tija ya kusaidia wafanyakazi. Kigezo cha wafanyakazi ishirini kuwa na uwezo wa kuunda chama cha wafanyakazi kimetumiwa vibaya na baadhi ya waajiri na kuwa sehemu ya wao kujinufaisha wao kupitia mgongo wa wafanyakazi.

Nne, ni changamoto ya **ada ya uwakala** yaani "agency shop fee" ambayo TUICO inaona kuwa inaleta matatizo katika utekelezaji wa shughuli hasa matumizi yake. Tunapendekeza kifungu hicho kisomeke kama ilivyokuwa kwenye sheria ya zamani yaani "union service charge" kwa tafsiri ya Kiswahili "ada ya huduma" ambapo Katibu Mkuu wa chama atapokea ada zote na kuzipangia majukumu kwa manufaa ya chama na wanachama wake. Na, TUICO iliiomba wizara itafute ufumbuzi wa kero ya malipo ya kiinua mgongo kwa wastaafu, wenye mkataba wa muda maalumu na wanaopunguzwa kazi.

Changamoto zingine ni pamoja na baadhi ya waajiri kuwa na sera zinazokiuka sheria za nchi ambazo zinachochea migogoro mingi sehemu za kazi na hivyo kukifanya TUICO kutumia muda na rasilimali nyingi katika kushughulikia migogoro hiyo. Janga la ugonjwa wa **Uviko-19** lilisababisha baadhi ya maeneo ya kazi kufungwa, upunguzwaji wa wafanyakazi na mishahara au kuachishwa kazi pamoja na baadhi ya wanachama kupoteza ajira kwa sababu ya kukosa vyeti vya kidato cha nne.

Lakini pia, **uunganishwaji wa baadhi ya taasisi** ikiwa ni pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii, benki za biashara na benki za umma ulisababisha baadhi ya wanachama kupoteza nafasi, marupurupu na stahiki zao. Pia, bado kuna uelewa mdogo kuhusu vyama vya wafanyakazi kwa baadhi ya waajiriwa. Kufungwa kwa baadhi ya maeneo ya kazi ambayo yamesababisha kupungua kwa idadi ya wanachama. Lakini pia, kuibuka kwa vyama kinzani (splinter unions) vyenye masilahi binafsi ambavyo vimekuwa vikiwarubuni wanachama kujitoa TUICO – hali hii inasababisha kudhoofisha mshikamano miongoni mwa wafanyakazi.

Mwelekeo Mpya

Kwa ujumla, tumepiga hatua nzuri katika nyanja za uhamasishaji, elimu, mikataba ya hali bora na utetezi kwa mfano, tumesimamia mgogoro katika kiwanda cha Mazava Fabrics and Production East Africa cha mkoani Morogoro. Lakini pia, Chama kimepanga kuimarisha na kukuza shughuli zake pamoja na kutoa huduma bora kwa wanachama wake. Vile vile, uwepo wa mfumo mpya wa mawasiliano wa TUICO pamoja na tovuti na mitandao yake ya kijamii, umeimarisha utendaji wa chama na kuwezesha utoaji wa huduma bora zaidi kwa wanachama.

Aidha, tumejipanga kuchochea ufikiwaji wa dira ya TUICO ambayo ni kuwa chama cha wafanyakazi ambacho ni imara, cha kidemokrasia na kinachotoa huduma bora kwa wanachama na wadau wake. Ni wito kwa wafanyakazi wote katika sekta za viwanda, biashara, fedha, huduma na ushauri kujifunza na kujiunga na TUICO leo. Mshikamano Daima!

TUICO KATIKA TAKWIMU

Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mwaka 2016-2020

Mikataba ya Hali Bora

Tumefunga mikataba 511 ya Hali Bora.
Mfano: 2019 TCC Plc Vs TUICO na 2020 Lake Cement Ltd. Vs TUICO

Semina na Mikutano

Tumefanya semina na mikutano 15,213 kwa wanachama na wafanyakazi maeneo ya kazi.

Utetezi wa Mashauri na Migogoro

Tumefanya utetezi na usimamizi wa migogoro na mashauri 7,007. Ya ana kwa ana, CMA, Mahakama za Wilaya/Mikoa, Mahakama Kuu (Kazi) na Mahakama Kuu.

Ziara Maeneo ya Kazi

Tumefanya ziara 18,279 kwenye maeneo mbalimbali ya kazi ili kukutana na wanachama na viongozi wetu ngazi za matawi.

Idadi ya Wanachama

Idadi ya Wanachama wa TUICO kwa kipindi cha mwaka 2016-2020 imeongezekwa kwa 30%

2016

2020

Kamati za Majadiliano

Tumefanikiwa kuunda kamati 528 za majadiliano katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini.

Uundaji wa Matawi

2016 tulikuwa na jumla ya matawi 1,487. 2020 tuna jumla ya matawi 2,362 kwenye sekta za viwanda, biashara, fedha na huduma na ushauri

Usanifu: Venance Majula, Afisa Habari TUICO

Tanzania Union of Industrial and Commercial Workers
P. O. Box 5680, Dar es salaam
Phone: +255 (0) 222 866 910 / 960, Fax: +255 (0) 222 866 911
E-mail: tuico2004@yahoo.com, Website: www.tuico.or.tz

tuicounion

Waziri Mhagama: Vyama vya Wafanyakazi Chachu Uboreshaji Mazingira ya Kazi

Waajiri nchini wametakiwa kutoogopa uwepo wa vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi kwa kuwa ndio fursa ya kutatua changamoto zinazojitokeza mahala pa kazi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama, Disemba 29, 2020 alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa Sita (6) wa Taifa wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) uliofanyika mjini Morogoro.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama, akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa Sita (6) wa Taifa wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) uliofanyika mjini Morogoro

Waziri Mhagama alisema TUICO pamoja na vyama vingine vya wafanyakazi nchini, vimekuwa tegemeo kwa wafanyakazi katika kulinda na kutetea haki, heshima na masilahi yao.

"Uwepo wa vyama vya wafanyakazi umekuwa ni nyenzo muhimu ambayo imeongeza tija na kujenga hali ya msukumo katika utendaji wa kazi wa wafanyakazi waliopo maeneo mbalimbali ya kazi nchini," alisema Mhe. Mhagama

Aidha, Waziri Mhagama alibainisha kuwa vyama vya wafanyakazi vimekuwa ni chachu ya uboreshwaji wa mazingira ya kazi ikiwa ni pamoja na uundwaji wa mabaraza ya kazi na ufungwaji wa mikataba ya hali bora kwenye maeneo ya kazi.

"Tumeshuhudia baadhi ya vyama vya wafanyakazi vimekuwa chachu katika kuhamasisha majadiliano baina ya waajiri na wafanyakazi katika kufunga mikataba ya hali bora ya kazi ambayo imekuwa ikiwanufaisha wanachama," alisema Mhe. Mhagama

Katika hatua nyingine, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA), Ndg. Tumaini Nyamhokya pamoja na mambo mengine, aliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutatua baadhi ya changamoto ambazo zimekuwa kilio kwa wafanyakazi wengi akitolea mfano punguzo la kodi "Pay as You Earn" ambalo limewanufaisha wafanyakazi kwenye sekta binafsi na sekta ya umma.

"Tunaahidi kuendelea kushirikiana na serikali pale tutakapoona kuna haja ya kutunga sheria sahihi za kazi na kuandaa sera nzuri za kuendeleza uchumi na manufaa kwa wafanyakazi," alisema Ndg. Sangeze

Naye, Kaimu Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi Bi. Pendo Berege alisema mkutano huo ni sehemu ya utekelezaji wa katiba na ndio sehemu pekee ya kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu chama.

"Ofisi ya Msajili inategemea kuona vyama vya wafanyakazi nchini vinaendelea kutekeleza katiba za vyama vyao, kutambua mipaka ya kiutendaji na kuendelea kutoa huduma bora kwa wanachama," alisema Bi. Berege

Mkutano huo Mkuu wa wa sita (6) wa Taifa wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) hufanyika mara moja katika miaka mitano na ni mkutano wa juu katika ufikiwaji wa maamuzi mbalimbali ya Chama.

TUICO Yashiriki Uzinduzi wa Mpango Kazi Kushughulikia Migogoro ya Kazi Nchini

Mwenyekiti wa TUICO Taifa Ndg. Paul Sangeze (Kulia), Katibu Mkuu Ndg. Boniface Nkakatisi (Katikati) na Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake TUCTA na Katibu wa TUICO Singida Bi. Rehema Ludanga (Kushoto) wakishiriki Uzinduzi wa Kliniki ya Utatuzi wa Migogoro katika sekta ya kazi na ajira. Jan. 2021, Morogoro.

Januari 29, 2021 serikali ilizindua Mpango Kazi wa Kusikiliza na Kushughulikia Malalamiko ya Wadau na Kikosi Kazi cha Ukaguzi Maalumu katika sekta ya kazi na ajira. Mpango huo ulizinduliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama katika hafla iliyofanyika ukumbi wa NSSF, Morogoro.

Akizungumza katika hafla hiyo Waziri Mhagama alisema lengo la mpango huo ni kuwawezesha wafanyakazi, waajiri na wananchi kwa ujumla kufahamu mamlaka sahihi zinazosimamia sheria zao na mamlaka sahihi zinazopokea malalamiko yao ni kupunguza migogoro ya wafanyakazi katika ulimwengu wa kazi.

"Mpango kazi una lengo la kuwawezesha wafanyakazi, waajiri na wananchi kwa ujumla kufahamu mamlaka sahihi, kwanza zinazosimamia sheria zao, na mamlaka sahihi zenye wajibu wa kupokea malalamiko yao," alisema Waziri Mhagama.

Aidha, Mhe. Mhagama alibainisha kuwa ujio wa mpango huo ambao unakuwa kliniki ya migogoro ya kazi, unaowaleta pamoja wafanyakazi kupitia TUCTA, waajiri kupitia ATE pamoja na serikali, sio mbadala wa mamlaka za usuluhishi zilizopo nchini, bali unalenga kubaini maeneo yenye changamoto na kutoa elimu sahihi ili kupata suluhu ya kudumu.

Katika uzinduzi wa kliniki hiyo ya kazi inayotarajiwa kufanya kazi mikoa yote nchini kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi, Mhe. Mhagama aliwataka wadau katika maeneo ya kazi kuaminiana na kuwa kitu kimoja ili kuhakikisha uzalishaji unakuwa wa ufanisi kwa manufaa ya pande zote zinazohusika.

"Kuna haja ya kubadilisha mindset [mtazamo], waajiri wasiwaogope wafanyakazi wala vyama vya wafanyakazi. Na vyama vya wafanyakazi visiwaogope waajiri. Hapo bado kuna gap [ombwe], waajiri wanaona vyama vya wafanyakazi kama ni maadui. Lakini ni lazima tujue sababu ni nini – tupate sababu hiyo tushughulike nayo," aliongeza Mhe. Mhagama.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Loata Ole Sanare aliishukuru Wizara ya Kazi kwa kupanga semina hiyo ifanyike mkoani Morogoro. Alisema hii ni fursa ya kutatua kero na changamoto za kazi zilizopo mkoani humo.

"Semina hii itaweza kutusaidia kuimarisha mahusiano kati ya wadau wote. Yaani kutatua shida na changamoto zote zitakazokuwepo," alisema Mhe. Ole Sanare

Rais wa Shirikisho la Wafanyakazi nchini (TUCTA) Ndg. Tumaini Nyamhokya aliwataka viongozi wa vyama wa wafanyakazi nchini kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha kwa wafanyakazi kuhusu mpango huu.

"Viongozi wa wafanyakazi tutoe elimu nzuri sana kwa wafanyakazi, wasije wakafiri hii kliniki ya kusikiliza na kutetea wafanyakazi, imekuja kuwa mbadala wa ule mfumo mzima wa ukataji wa rufaa za wafanyakazi. Kwa hiyo, ipo CMA, ipo Mahakama Kuu - Lakini kwenye hatua za awali kabla tatizo halijawa kubwa, basi wafike kwenye kliniki hii. Huenda tatizo likatatuliwa kabla halijafika mahakamani," alitanabaisha Nyamhokya

Naye Dkt. Aggrey Mlimuka - Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) alisema mpango huu unafaida kwa pande zote tatu.

"Amani sehemu za kazi inatunufaisha wote. Wafanyakazi watapata huduma zaidi, waajiri watapata kipato zaidi, serikali nayo itapata kipato zaidi ili ifanye miradi yake zaidi," alisema Dkt. Mlimuka.

Kwa upande wake Ndg. Maridadi Phanuel, Mratibu wa Taifa wa Sheria za Kazi - Shirika la Kazi Duniani (ILO-Tanzania), kwa niaba ya Mkurugenzi wa shirika hilo ukanda wa Afrika Mashariki, alisema ILO itaendelea kushirikiana na wadau wote nchini ili kuhakikisha kunakuwa na kazi zenye staha.

"Utatuzi wa migogoro unatakiwa kuwa wa wakati na kwa kufuata utaratibu ili kuhakikisha pande husika wanakuwa na mahusiano mema.

Kuweka namna ya kupokea malalamiko sehemu za kazi na kuhakikisha malalamiko hayo yanashugulikiwa ipasavyo na kwa utaratibu ili kuhakikisha kunakuwa na kazi za staha," alisema Ndg. Maridadi

Miongoni mwa waliohudhuria uzinduzi wa mpango huo ni pamoja na Katibu Mkuu wa TUCTA Ndg. Said Wamba, Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa TUICO Ndg. Paul Sangeze na Ndg. Boniface Nkakatisi, mtawalia - pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake TUCTA ambaye pia ni Katibu wa TUICO Singida, Bi Rehema Ludanga.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mh. Jenista Mhagama akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Mpango Kazi wa kushughulikia na kusikiliza malalamiko ya wadau na kikosi kazi cha cha ukaguzi maalumu katika sekta ya kazi na ajira, Jan 29, 2021, Morogoro.

M A T U K I O K A

Mkutano Mkuu wa Sita wa TUICO Taifa,
Disemba 29, 2020 – Morogoro

T I K A P I C H A

Mkutano Mkuu wa Sita wa TUICO Taifa,

Disemba 29, 2020 – Morogoro

TUICO Yafanya Uchaguzi Mkuu

Mwenyekiti wa TUICO Taifa Ndg. Paul Sangeze (Kulia), Katibu Mkuu Ndg. Boniface Nkakatisi (Kushoto) wakiwa wameshikilia mataji baada ya kutangazwa washindi katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Disemba 29, 2020, Morogoro.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Sita wa Taifa wa TUICO uliofanyika Disemba 29, 2020 Mjini Morogoro, walimchagua Ndg. Paul Sangeze kuwa Mwenyekiti wa TUICO Taifa kwa kipindi cha mwaka 2021-2025.

Akitoa salamu za shukurani kwa wajumbe wa Mkutano huo, Sangeze alisisitiza umuhimu wa umoja kwenye chama ili kiweze kufikia malengo yake.

"Ni wakati sasa wa kujenga umoja ndani ya chama ili tuendelee kupigania masilahi ya wafanyakazi ambao kimsingi ndio tunawatumikia" alisema.

Katika hatua nyingine, Wajumbe wa Mkutano huo walimchagua Ndg. Boniface Nkakatisi kuwa Katibu Mkuu wa TUICO Taifa kwa kipindi cha mwaka 2021-2025.

Ndg. Nkakatisi alisema ataongeza juhudi zaidi katika utoaji wa elimu kwa wanachama na wafanyakazi kwa ujumla ikiwa ni katika kujibu miongoni mwa hoja zilizoibuka kutoka kwa wajumbe wa Mkutano huo.

"Nimesikia miongoni mwenu mkisisitiza elimu. Tutaanza na elimu kwa wanachama wetu ili wawe na ujasiri zaidi katika maeneo yao ya kazi," alisema

Wengine waliochaguliwa ni pamoja na Wajumbe wa Baraza Kuu, Wajumbe wa Kamati ya Utendaji TUICO Taifa na Wajumbe wa TUICO katika Shirikisho (TUCTA).

Katika Uchaguzi huo Mkuu ulioshuhudiwa na Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi Bi. Pendo Berege, Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi (CMA), na waalikwa wengine, Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa TUICO Taifa walitetea nafasi zao ndani ya Chama ambazo wamezitumikia kwa miaka mitano iliyopita.

Nguvu ya Mshikamano Katika Kupigania Haki za Mfanyakazi

Vyama vya wafanyakazi ni asasi muhimu katika ulimwengu wa kazi. Vyama vya wafanyakazi ni daraja baina ya tabaka la wafanyakazi, waajiri na serikali. Kwa sababu malengo ya wafanyakazi na waajiri hayakubaliani, migogoro baina ya tabaka mbili hizi ni vitu vinavyotarajiwa. Vyama vya wafanyakazi hutumiwa na wafanyakazi wenyewe kama chombo chao cha utetezi.

Katibu Mkuu wa TUICO Taifa Ndg. Yohana Nkakatisi (wa pili kulia, mbele), Mkurugenzi Mkuu wa Lake Cement Limited Ndg. Bwiswajeet Malik (wa tatu kulia, mbele) na Naibu Katibu Mkuu wa TUICO Ndg. Tamim Salele (Kushoto), baada ya kusaini Mkataba wa Hali Bora kati ya Lake Cement na TUICO. Agosti, 2020, Dar es Salaam.

Wafanyakazi wanakuwa na matatizo kadhaa katika sehemu zao za kazi. Matatizo hayo hayatokani na amri ya Mungu. Hivyo wafanyakazi hawana budi kuyatatua ili kuondoa vikwazo katika shughuli zao za kazi na kuinua hali zao za maisha wakiwa wafanyakazi. Kwa mfano, katika kiwanda kuna mtaji, utawala au uongozi na nguvukazi. Kila kimoja kinajitegemea ingawa katika uendeshaji ama utendaji wa kazi vinategemeana na malengo yake pia yanatofautiana.

Mwekezaji ambaye ndiye wenye mtaji, lengo lake ni kupata faida kubwa kadri inavyowezekana ambapo utawala upo pale kulinda na kukuza maslahi hayo na wafanyakazi huuza nguvu zao. Katika mazingira hayo, wafanyakazi huishia kunyonywa. Wafanyakazi kwa hivyo wanastahiki malipo ya haki na usawa kwa nguvukazi wanayoitoa. Uwezo wa mfanyakazi mmoja mmoja kupigania haki yake ni mdogo.

Hakuna mafanikio ya maana anayoweza kupata mfanyakazi peke yake katika kupigania haki yake. Ni kwa kupitia chama cha wafanyakazi pekee kinachounganisha pamoja nguvu za wafanyakazi wote kinachoweza kuinua heshima ya wafanyakazi mbele ya waajiri, na kupigania ujira utakaomwezesha mfanyakazi kuishi, kupata hali bora ya maisha, na kupata marupurupu mengine.

Hayo hasa ndiyo yaliyoleta haja ya wafanyakazi kujiunga pamoja na kuibuka na vyama vya wafanyakazi. Kuunda vyama vya wafanyakazi ni haki ya msingi ya wafanyakazi wenyewe. Jiunge na Chama cha Wafanyakazi sasa.

Mkuu wa Sekta ya Huduma na Ushauri TUICO, Margaret Ndagile (Mwenye miwani katikati), Mkuu wa Idara ya Elimu, Fredrick Mng'ong'o (katikati) wakiwa na watumishi wa afya kutoka ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mufindi na viongozi wa vijiji wakati wa tathmini ya zoezi la Ushauri Nasaha na Upimaji wa Afya kwenye kiwanda cha karatasi Mufindi, Iringa, Novemba, 2020.

Sangeze: Ni Wakati wa Kuwajibika Zaidi

Mwenyekiti wa TUICO Taifa Ndg. Paul Sangeze akifungua kikao cha kutathmini na kupanga Mpango Mkakati wa TUICO kwa mwaka 2021-2025, Morogoro, Januari, 2021.

Mweyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) Ndg. Paul Sangeze, Jumatano, Januari 27, 2021 alifungua kikao cha kutathmini na kupanga mpango mkakati wa Chama.

Akifungua kikao hicho, Sangeze aliwataka watumishi wote wakiwemo makatibu wa sekta, idara na vitengo; makatibu wa kanda na mikoa; pamoja na watendaji wote kuhakikisha wanatimiza majukumu yao kwa ufanisi katika utekelezaji wa mpango kazi wa TUICO unaopangwa.

"Kupanga mpango ni jambo moja na utekelezaji ni suala jingine. Hatupaswi hata kidogo kufumbia macho pale inapoonekana mmoja wetu anahujumu utekelezaji wa mpango kazi utakaopangwa kwa uzembe na kwa kutotimiza wajibu," alisema Sangeze.

Sangeze aliongeza kuwa mahitaji ya chama kiuendeshaji ni makubwa. Wanachama na watendaji wana matarajio makubwa kimafanikio kutoka TUICO. Hivyo alisisitiza umoja, mshikamano, uwazi na uwajibikaji kwa kila mmoja ili kuakisi mwelekeo na mahitaji ya chama.

"Tuanze pamoja kwa malengo makubwa na tumalize pamoja kwa mafanikio makubwa," aliongeza Sangeze.

Kwenye kikao hicho cha siku tatu, kilichofanyika mkoani Morogoro, pamoja na mambo mengine wajumbe walifanya tathmini ya mpango mkakati wa TUICO uliomalizika Disemba 2020 na kupanga mpango kazi mwingine kwa mwaka 2021-2025.

"Hiki ni kikao muhimu sana kwa chama chetu. Hapa tutafanya tathmini ya mpango mkakati wa Julai-Disemba, 2020 na kupanga mpango mkakati wa miaka mitano 2021-2025 na mpango mkakati wa Januari-Disemba, 2021. Kwa hiyo wajumbe tuwe wawazi na wakweli," alisema Naibu Katibu Mkuu (TUICO), Ndg. Tamim Salehe.

Kwa niaba ya wajumbe, Katibu wa TUICO Mkoa wa Iringa na Njombe Ndg. Karim Bachalla alitoa salamu za wajumbe ambapo alisema wanakubaliana na maneno ya Mwenyekiti na wako tayari kuhakikisha chama kinanufaikia na mpango mkakati uliopangwa.

"Tunakubalina na wewe kabisa, kwamba chama kutokuwa na mpango mkakati ni sawa na kuwa mfu. Kwa hiyo tutapanga mpango mkakati utakaokuwa na manufaa kwa chama.

Tunaendelea kusisitiza, tutapanga mambo yenye kutekelezeka kwa manufaa ya wafanyakazi," alisema Bachalla

Kwa upande mwingine, Sangeze aliwapongeza makatibu na watendaji wote kwa kazi nzuri iliyopelekea mafanikio ya kuridhisha ambayo yamekifikisha chama hapa kilipo.

KUT Yajadili Bajeti ya TUICO 2021

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya TUICO Taifa baada ya Kikao cha kujadili bajeti ya Chama kwa mwaka 2021 kilichofanyika Januari, 2021, Morogoro.

Kamati ya Utendaji TUICO Taifa (KUT) Jumanne, Januari 26, 2021 ilipitia na kujadili bajeti a Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) kwa mwaka 2021.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika Morogoro, Naibu Katibu Mkuu wa TUICO Taifa Ndg. Tamim Salehe ambaye pia ni Mjumbe wa KUT ameeleza baadhi ya changamoto zilizojitokeza mwaka 2020.

"Mnafahamu kwamba kumekuwa na changamoto ya Uviko-19. Kuna makampuni mengi yalifunga, wafanyakazi walifanya kazi wakiwa nyumbani na wengine walipunguzwa kabisa," alisema Ndg. Tamim

Akifunga kikao hicho Mwenyekiti wa TUICO Taifa Ndg. Paul Sangeze aliwashukuru Wajumbe wa KUT na kuwatakia safari njema wakati wakirejea kwenye maeneo yao ya kazi,"

"Kwanza nimshukuru Mungu. Ninawashukuru wajumbe wote kwa michango yenu. Nimshukuru Katibu Mkuu na Wajumbe wake kwa semina ya jana. Naamini ile semina imetupeleka mahala," alisema Ndg. Sangeze.

Aidha, Sangeze alisisitiza umoja na mshikamano ndani ya TUICO huku akikipongeza chama na Mkutano Mkuu kwani idadi kubwa ya wajumbe wa KUT ni wanawake. Alisema uwepo wa vijana na wanawake kwenye KUT ni miongoni mwa mageuzi makubwa katika historia ya vyama vya wafanyakazi hususani TUICO.

"Tuishi kama ndugu wanaonia mamoja. Miaka mitano ni mingi mno na ni michache mno. Naamini tukianza vizuri, tutamaliza vizuri. KUT ina akina mama saba na akina baba watano. Hii ni ishara fulani.

Haijawahi kutokea katika historia ya TUICO. Ni hatua kubwa sana," aliongeza Ndg. Sangeze

Kwa mwaka 2021, TUICO imejipanga kufanya uhamasishaji, elimu, mikataba ya hali bora, utetezi zaidi, lakini pia, kuimarisha na kukuza shughuli zake pamoja na kutoa huduma bora kwa wanachama ili ifikie dhamira yake ambayo ni kuwa chama imara na cha kidemokrasia kinachotoa huduma bora kwa Wanachama na Wadau wake.

TUICO Yafanya Uchaguzi wa Kamati za Vijana na Wanawake

Wajumbe wa Kamati ya Vijana TUICO Taifa baada ya uchaguzi wa Kamati hiyo Disemba, 2020, Morogoro.

Disemba 17 na 18, 2020, TUICO ilifanya uchaguzi wa Kamati zake mbili; Kamati ya Vijana na Kamati ya Wanawake Taifa. Katika uchaguzi wa Kamati ya Vijana, Ndg. Allen Lyimo alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana huku Bi. Zeralucy Masanja akichaguliwa kuwa wa Mwenyekiti Kamati ya Wanawake; kwa kipindi cha mwaka 2021-2025.

Katika zoezi hilo, Mwenyekiti wa TUICO Taifa Ndg. Paul Sangeze aliwaasa viongozi waliochaguliwa kujenga umoja na mshikamano ndani ya Chama ili TUICO iendelee kudumu.

Aliongeza kuwa wanawake na vijana wana nafasi kubwa ya kubadilisha mtazamo wa wanawake na vijana wengine nchini kuhusu vyama vya wafanyakazi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa TUICO Taifa, Ndg. Boniface Nkakatisi alisema uongozi ni utumishi hivyo ni lazima viongozi wanaochaguliwa ndani ya chama wawe watumishi wa wengine ili chama kiendelee kudumu. Nkakatisi alisisitiza kuwa, zama zimebadiliaka, ni lazima vijana wafanye mambo yao kwa hoja katika suala zima la kupigania, kutetea na kulinda haki, heshima na masilahi ya wafanyakazi.

Akiwashukuru wajumbe wa Mkutano wa Kamati ya Vijana, Allen ambaye ni mfanyakazi wa kiwanda cha Sunflag Limited cha Arusha, alisema atajikita kufanya mambo yanayoonekana na kutumia uzoefu alionao kuwainua vijana ndani ya chama sambamba kuwahamasisha wengine ambao ni wafanyakazi kujiunga na TUICO.

Naye, Bi. Zeralucy, mfanyakazi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambaye alifanikiwa kutetea nafasi yake kwa kipindi cha pili mfululizo aliahidi kupigania masilahi ya wafanyakazi wanawake ndani ya TUICO.

Wajumbe wa Kamati ya Wanawake TUICO Taifa baada ya Uchaguzi - Disemba, 2020, Morogoro.

Karibuni Ofisini!

Hafla ya Kuwakaribisha na Kuwapongeza Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa TUICO Taifa Ndg. Paul Sangeze na Ndg. Boniface Nkakatisi zilizofanyika Januari 4 na 5, 2021 kwenye Ofisi za TUICO Makao Makuu Ilala, Dar es Salaam.

Ndg. Sangeze na Ndg. Nkakatisi walichaguliwa kwa mara nyingine na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa TUICO Taifa Disemba 29, 2020 kuwa Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa TUICO hadi 2025.

Mfanyakazi wa Karne ya 21

Wakati idadi ya watu wanaofanya kazi barani Afrika inatarajiwa kuongezeka kwa watu milioni 450 ifikapo 2035 (sasa ni milioni 440 {Benki ya Dunia}), uchumi wa kidigitali pia unazidi kukua. Hapa tunamaanisha, uchumi ambao unategemea teknolojia ya kompyuta. Kwa maneno mengine – uchumi wa kimtandao.

Kwa maana hiyo tunaweza kusema kuwa mfanyakazi wa karne ya 21, ni 'binadamu mpya' kwenye uchumi mpya. Hii ni mara ya kwanza katika historia ya ulimwengu wa kazi, ambapo tuna ufikiaji mkubwa wa zana za kiteknolojia ambazo zinampa kila mmoja wetu sauti nje ya kuta za makampuni au taasisi za kazi. Lakini pia tunapata taarifa na kuna mwingiliano baina yetu kikazi.

Siku hizi kila mmoja anaweza kutumia mtandao kutafuta kazi, kusoma sheria na kanuni mbalimbali za kazi lakini pia tunasoma maoni ya watu wengine mtandaoni. Hii inamaanisha kwamba, nje ya mazingira ya kazi, tayari tuna sauti na tunaweza kushiriki hisia zetu wakati wowote – nayo ni mtandao. Mwajiriwa unaweza kujua haki na majukumu yako kisheria kwa kutumia mtandao wa intaneti hata kama kazini kwako hakuna hizo sheria.

Kwa mfano, janga la Uviko-19 limetufundisha sisi sote kwamba licha ya kuwa na ulimwengu wa mwili, pia tuna ulimwengu mtandao na tunahitaji kuwa na uelewa wa matumizi ya zana za kidigitali. Ni wakati wa janga hili, karibu kila kampuni imetumia majukwaa ya mikutano ya video kama Zoom, Skype au Hangouts za Google kufanya mikutano na watu wamefanya kazi wakiwa nyumbani. Vyama vya wafanyakazi pia vilitumia mtandao kufanya shughuli tofauti za uhamasishaji na elimu kwa wafanyakazi.

Hivyo, katika karne hii ya 21, tunahitaji kujitenga na mifumo tuliyoizoea ya kimenejimenti ili tuweze kukonga mioyo na akili za wafanyakazi ambao wanataka kufanya kazi zao za maisha. Kuhusu wale ambao bado hawajapata elimu ya kidigitali, sisi sote tunawajibika kuchambua mwenendo wa kazi duniani na kuwaimarisha wafanyakazi wote kwa kile kinachotokea katika ulimwengu wa kazi na maisha - mambo yanabadilika jamani.

Haya yote yatafanikiwa endapo kutakuwa na uwekezaji wa mitaji iliyolengwa vizuri kwenye rasilimali watu na vitu. Lakini pia sera zinazokuza ushindani, elimu ya kidigitali pamoja na uzalishaji wenye tija. Nguvu kazi kubwa ya Afrika ambayo ni vijana, ina uwezo wa kubadilisha bara hili kwa kiwango kikubwa na kusababisha ajira zenye staha kwa wote. Mshikamano Daima.

WAJUMBE WA BARAZA KUU TUICO

WADHIFA	NA	JINA	JINSI		SEHEMU YA KAZI
Mwenyekiti wa TUICO Taifa	1	Paul Edward Sangeze	Me		Coims Development
Katibu Mkuu	2	Boniface Yohana Nkakatisi	Me		TUICO Makao Makuu
Naibu Katibu Mkuu	3	Tamim Salehe	Me		TUICO Makao Makuu
Mkuu wa Sekta – Biashara	4	Peles Jonathan	Me		TUICO Makao Makuu
Mkuu wa Sekta – Fedha	5	Willy Kibona	Me		TUICO Makao Makuu
Mkuu wa Sekta – H/Ushauri	6	Margaret Ndagile		Ke	TUICO Makao Makuu
Wajumbe 12 wa Baraza Kuu	7	Fidelis F. Nsalamba	Me		SBC(T) Ltd – Ilala
	8	Magdalena Samkhumbi		Ke	KIUTA – Temeke
	9	Mathias Otto Nchimbi	Me		Tancoal - Ruvuma
	10	Asha Mtola Kombo		Ke	TANESCO - Temeke
	11	Haruna Kipanga Haruna	Me		TANESCO - Kasulu
	12	Theopist Gabriel Semanini	Me		TANESCO - Iringa
	13	Arafa Faki Hamisi		Ke	NMB PLC- Songea
	14	Nsengiyumva James Msechu	Me		NSSF – Moshi
	15	Nsesheye Godfrey Mboma		Ke	TPB Bank - Ilala
	16	Juma Nassoro Mtoro	Me		DAWASA - Kinondoni
	17	Mwinga Mazwile Luhoyo		Ke	Masoko Kariakoo – Ilala
	18	Yusuph Mohamed Simbaulanga	Me		YMS Electrical - Mwanza
Wajumbe 12 wa Kamati ya Utendaji Taifa	19	Abdallah Salehe Msese	Me		Shelys Pharmaceutical - Kinondoni
	20	Dismas Hubert Mgalla	Me		21 Century Textile – Morogoro
	21	Winnie Shangali Swai		Ke	Bonite Bottlers - Kilimanjaro
	22	Enna Frank Ringo		Ke	TANESCO-Moshi
	23	Nazir Abdul Ismail	Me		TANESCO -Wanging` ombe Iringa
	24	Zamda Masoud Mfaume		Ke	AICC - Arusha
	25	Lizzy Elibariki Msechu		Ke	CRDB – Chamwino Dodoma
	26	Mbwana Ally Selemani	Me		NSSF Mafinga Iringa
	27	Mzelela Makwaya	Me		TPB Bank PLC Musoma Mara
	28	Agness Paul Njau		Ke	AUWSA – Arusha
	29	Mwanaidi Hassan Bakari		Ke	LUWASA – Lindi
	30	Zainabu Rashid Mapila		Ke	MTUWASA - Mtwara
Kanda ya Dar es salaam	31	Peter J. Mkumbi	Me		Tantrade
Kanda ya Mashariki	32	Canlidy P. Ngowi	Me		DAWASA - Pwani
Kanda ya Kaskazini	33	Patrick Mbelwa	Me		Tanga Cement
Kanda ya Kati	34	Ramadhani Butallah	Me		TANESCO Dododma
Kanda ya Ziwa	35	Thadei Mapunda	Me		TANESCO Mwanza
Kanda ya Magharibi	36	Victor S. Mbesigwe	Me		NSSF Tabota
Kanda ya Nyanda za Juu Kusini	37	Daudi A. Mpolya	Me		TANESCO Mkoa
Kanda ya Kusini	38	Mukh Seif Makota		Ke	MTUWASA - Mtwara
Kanda ya Dar es salaam	39	Innocent Benjamin Alute	Me		TUICO Ilala
Kanda ya Mashariki	40	Boniface Nyenyembe	Me		TUICO Morogoro
Kanda ya Kaskazini	41	Renatus Chimola	Me		TUICO Arusha
Kanda ya Kati	42	Rajabu Jaha	Me		TUICO Dodoma
Kanda ya Ziwa	43	Martin Wawa	Me		TUICO Mwanza
Kanda ya Magharibi	44	Christopher Malechela	Me		TUICO Tabora
Kanda ya Nyanda za Juu Kusini	45	Merboth Kapinga	Me		TUICO Mbeya
Kanda ya Kusini	46	Guerinous Mgima	Me		TUICO Ruvuma
Mwenyekiti kamati ya Wanawake Taifa	47	Zeralucy Masanja		Ke	Benki Kuu -HQS
Mwenyekiti Kamati ya Vijana Taifa	48	Allen Michael Lyimo	Me		Sunflag Ltd - Arusha
Wawakilishi Zanzibar	49	Nuhu Namanje	Me		Benki Kuu -Zanzibar
	50	Salum Chaurembo	Me		Benki Kuu -Zanzibar
Wadhamini wa Chama	51	Abdukarim Mtoni	Me		Kipwele Security
	52	Laura Hyera		Ke	

Ilala Sharif Shamba | S.L.P. 5680, Dar es Salaam.
Simu: +255 22 2866910, 2866959/60 | Faksi: +255 22 2866911
Barua pepe: tuico2004@yahoo.com

Info: info@tuico.or.tz | Facebook: @tuicounion | Instagram: @tuicounion |
Twitter: @tuicounion | YouTube: TUICO UNION

Jenga Chama Imara. Imarisha Mshikamano